**NYUMBA YA HAKI YA ULIMWENGU**

**31 Desemba 2025**

Kwa Kongamano la Bodi za Washauri wa Bara

Marafiki wapendwa sana,

Awamu ya kwanza ya Mpango wa Miaka Tisa imetoa mwanga juu ya nguvu kubwa za jumuiya ya Kibahá'í. Nguvu na ari isiyo na kifano ambayo kwayo Mpango ulizinduliwa, katika mikusanyiko zaidi ya 10,000 ya Wabahá'í na marafiki wenye shauku, iliongeza kwa haraka utambuzi wa malengo na sifa yake ya kipekee. Hatua ya haraka ilifuatia. Tunatarajia kwamba hadi kufikia Riḍván kutakuwa na klasta ambapo hatua ya tatu itakauwa imevukwa katika takribani nusu ya nchi na maeneo 160 ambapo, mwanzoni mwa Mpango, bado hakukuwa na klasta kama hiyo—haya ni mafanikio ya kushangaza. Matokeo yake, tajiriba ya thamani imepatikana, hasa kupitia juhudi za kujitoa za idadi ya kuvutia ya watu walioinuka kama sehemu ya mkakati wa utangulizi ulioratibiwa. Wakati huo huo, umakinifu maalum umeelekezwa katika nchi zote kwa klasta za hatua ya tatu, na kwa hiyo, wigo wa ujifunzaji umepiga hatua kubwa na nguvu ya Imani ya ujengaji jamii inazidi kudhihirika. Nyingi ya klasta hizi zinakuwa kama bwawa la maarifa na rasilimali kwa klasta zinazozizunguka, na hili linathibitisha kuwa muhimu kwa ajili ya mchakato wa ukuaji kila mahali. Kwa hakika, kasi ya mjongeo wa klasta kuvuka hatua ya kwanza, ya pili, na ya tatu unahitaji kwamba mtindo huu uimarishwe na kuigwa kwa mapana. Ingawa tunafurahia maendeleo yaliyopatikana, ni dhahiri kwamba kazi nzito kabisa ipo mbele ikiwa tu kila jumuiya ya Kibahá'í ya kitaifa itahitaji kutimiza malengo ya mjongeo wa klasta iliyojiwekea Mpango ulipoanza. Kuna hitaji la haraka la kukuza kwa mapana zaidi stadi zihitajikazo kushadidisha program ya ukuaji. Mahali muhimu pa kurejelea kwa kazi hii—na kwa kazi zote za Mpango wa Miaka Tisa—bila shaka pataendelea kuwa ujumbe wetu wa 30 Desemba 2021, lakini ndani ya kurasa hizi chache, tutajaribu kuwasilisha baadhi ya umaizi ulioibuka kutokana na juhudi za jumuiya, asasi na watu binafsi kadiri walivyokuwa wakitekeleza Mpango.

*

Katika klasta na katika ujirani na vijiji ambako maendeleo makubwa yamepatikana, haidhuru ni wapi pa kuanzia, kigezo cha msingi kimekuwa uwezo wa marafiki mashinani kujifunza pamoja, wakichanganya umaizi uliopatikana kutokana na tajiriba yao wenyewe na ule wa jumuiya zilizopiga hatua zaidi za karibu au mbali, bila kuwa na fikra yoyote ya kutumia fomula iliyowekwa. Ingawa vipengele vya msingi vya program ya ukuaji—shabaha yake, kanuni zake ziongozazo, na vyombo vyake vya kimsingi—ni sawa kila mahali, ukuaji ni mchakato wa njia ya asili, siyo ule wa kimakanika. Katika mchakato kama huo, maendeleo hutegemea kila wakati kudumisha uelewa dhahiri wa vipaumbele vinavyohusu mahali husika na, kama tulivyosisitiza katika ujumbe wetu kwa kongamano lenu la 2021, kusoma uhalisia ubadilikao na kutumia mbinu zifaazo kulingana na hali za mahali.

Hatua ya tatu ni kipimo cha safari ambayo mwanzo wake unaeleweka vizuri. Mara tu inapovukwa, klasta ambako maendeleo yameimarishwa zaweza kuonekana kuwa na vipengele muhimu vinavyofanana. Programu za taasisi zinasaidiwa na bwawa kubwa kiasi na lipanukalo la rasilimali watu. Juhudi zinafanywa ili kuwezesha ujirani na vijiji zaidi kudumisha shughuli shadidi. Kuna uwezo wa kukumbatia idadi kubwa na kusimamia utata uongezekao kupitia mipangilio yote miwili; rasmi na isiyo rasmi. Muhimu zaidi, katika klasta hizi, umakinifu thabiti unatolewa kwa kudumisha duru zenye ufanisi, ili kuwe na mdundo wa mara kwa mara wa kusoma, kushauriana, kutenda na kutafakari ambao kwa huo jumuiya huongeza uwezo wake wa kukua na kuchangia kwenye maendeleo ya jumuiya ambayo ni sehemu yake. Duru hizi hujumuisha vipindi vyenye nguvu maalum, kuongeza nguvu inayosukuma ushiriki wa duara pana zaidi kadiri iwezekanavyo la marafiki. Shughuli za jumuiya kama vile sherehe za kifamilia, kambi za vijana chipukizi, miradi ya huduma, jitihada za sanaa, na mipango ya ufundishaji wa pamoja zinaendelea kulingana na midundo yao husika. Nafasi za tafakari huwaleta pamoja marafiki wengi, na matumizi ya nafasi kama hizo ni yenye umakini na ya makusudi—kuna uelewa kwamba ubora na manufaa ya tafakari hupimwa kwa hatua za makusudi zinazotokana nayo. Kutoka klasta hizi, rasilimali hutiririka kwenda klasta zinazozizunguka ili kuwasaidia marafiki huko ili kuchapuza maendeleo.

Tumechunguza kwa umakini maalum jinsi ari ya jumuiya iliyo dhahiri inavyoweza kuhisiwa zaidi miongoni mwa wale wote wanaohusika katika ruwaza ya shughuli katika klasta za hatua ya tatu, hata kama haina nguvu sana katika jamii pana. Mara nyingi huoneshwa kama hisia ya kuwa sehemu ya kitu na utambuzi wa jitihada za pamoja na kusaidia. Haya pamoja na maendeleo mengine katika kiwango cha utamaduni yanazidi hasa kudhihirika katika vituo vya klasta zenye shughuli shadidi—si tu pale ambapo ushiriki unaweza kupimwa kama sehemu kubwa ya idadi ya watu, bali katika ujirani au kijiji chochote ambako idadi kubwa inavutiwa na programu na shughuli za jumuiya. Kuna ongezeko vile vile katika mipangilio mbalimbali ya ushirikiano, ambayo inafanya mengi kujenga au kuunda upya utambulisho wa pamoja wa kijamii na kusudi la pamoja. Mipangilio hii hujumuisha makundi ya familia na kaya tuliyoyataja mwaka 2021 na pia makundi mengine ya kiasili kama vile wanawake au vijana, wakulima au walimu, na wahuishaji au walimu wa madarasa ya watoto, mara nyingi wakiwa na mtandao saidizi wa marafiki. Makundi ya aina hii huanza kupanga juhudi zao wenyewe kuboresha baadhi ya vipengele vya maisha ya jumuiya, na kukuza ushiriki mpana zaidi katika juhudi hizo. Kwa maneno mengine, wanasaidia ukuaji na maendeleo ya jumuiya kuwa endelevu, na wanafanya hivyo bila haja matabaka mapya ya muundo wa kiutawala. Hili lina matokeo makubwa. Hii huonesha uwezo unaoibuka wa jumuiya kuwa mhusika mkuu anayeonekana katika Mpango. Ikiimarishwa na imani kamili na mwongozo wa upendo wa asasi, jumuiya huongoza mwelekeo wa maendeleo yake kwa ubunifu na ustadi, na kuchunguza jinsi kanuni zilizomo katika Ufunuo wa Bahá'u'lláh zinavyoweza kutumika kwa masuala yanayoikabili katika uhalisia wake wa sasa.

Haishangazi kwamba shughuli zenye mlengo wa kijamii tuliyoieleza kwenu mwaka 2021 mara nyingi hutokana na mipangilio ya ushirikiano iliyotajwa hapo juu. Jitihada hizi za kawaida lakini endelevu za shughuli za kijamii huwakilisha eneo la jitihada ambalo, bila shaka, limekuwa likidokezwa katika mpango wa ukuaji tangu mwanzo; hata katika kozi za awali kabisa za taasisi, uwezo hujengwa kwa ajili ya vitendo ambavyo huchangia kwenye hali bora ya ulimwengu na kwa ajili ya mazungumzo yenye maana juu ya masuala yenye umuhimu wa kijamii. Katika miaka minne iliyopita, jitihada kadhaa zenye mlengo wa kijamii zinazotokana na shughuli za Mpango zimeongezeka sana. Baadhi pia zimetokana na hamasa, mafunzo na msaada wa shirika lenye uvuvio wa Kibahá'í. Jitihada zote hizi zina uwezekano mkubwa wa kuibuka katika maeneo ambako mchakato wa ujengaji jumuiya umeendelea kwa kiasi kikubwa,

na tunathamini mchango ambao nyinyi na wasaidizi wenu, pamoja na Mabaraza ya Kiroho ya Mahali, mlioutoa kwa jitihada hizo. Hali zilizowezesha haya kutokea na kushamiri katika mazingira mbalimbali kote ulimwenguni yanaendelea kuchunguzwa kwa makini na Shirika la Kibahá'í la Maendeleo la Kimataifa, ikiwemo jinsi, baada ya muda, baadhi ya jitihada hizi zinavyopiga hatua na kuwa mashirika yenye mlengo wa kijamii.

Kwenye kiini cha maendeleo ya jumuiya, bila shaka, kuna mchakato wa taasisi. Maadam uwezo wa kufanya kazi na idadi kubwa katika klasta bado ungali unajengwa, ni jambo la kawaida kwa juhudi za taasisi kumakinikia kwa kiasi kikubwa hasa katika kukuza rasilimali watu wanaoweza kutekeleza vitendo mahsusi vya huduma. Lakini baada ya muda, baada ya kuvukwa kwa hatua ya tatu na vituo fulani vya shughuli shadidi kuimarika, taasisi pia itahitaji kutafakari kwa kina zaidi jinsi ya kutoa kimpangilio na kwa ufanisi programu inazotoa tangu utotoni hadi utu uzima, na uenezaji wa programu hizi katika sehemu zingine za klasta. Madarasa ya watoto katika madaraja yote yanaanzishwa, vitabu kadhaa vinavyosomwa na vikundi vya vijana chipukizi huongezeka, na ushiriki katika program zote mbili hudumishwa mwaka baada ya mwaka, ambapo vyote hivi huzipa shughuli hizi kiwango cha juu zaidi cha urasimishaji. Mara nyingi, maendeleo haya hutegemea huduma itolewayo na kundi liongezekalo la vijana. Juhudi za taasisi pole pole hushamirishwa na jitihada za ziada za kielimu kwa ajili ya maendeleo ya watu, kama vile program zinazotumia nyenzo zenye uvuvio wa Kibahá'í, hali kadhalika kozi zinazopatikana katika jamii pana, au hata, kwa baadhi ya maeneo, shule ya jamii. Katika ujumbe wetu wa 30 Desemba 2021, tulielezea tumaini kwamba umakinifu utatolewa kwa kuwasaidia vijana kupata fursa za kielimu, na tumefurahi kuona hitaji hili likitimizwa kwa namna mbalimbali, ikiwemo mafunzo ya baada ya shule na msaada kwa vijana wanaotaka kujiunga na elimu ya juu. Kadiri njia pana ya kielimu inavyoanza kupata umbo, jumuiya hujiona kuwa na jukumu kubwa zaidi la kumchochea na kumhamasisha kila mmoja wa wana-jumuiya wake, hususan vijana, kuendelea katika njia hiyo kwa kutafuta ukuaji wa kiroho na kiakili.

Tumetambua manufaa yatokanayo na kukuza ufahamu katika jamii pana wa thamani ya kielimu ya program za taasisi. Hii imehusisha juhudi za kuwafikia wazazi na ndugu wa watoto na vijana chipukizi, na pia maafisa na waelimishaji wakuu ambao Wabahá'í wanashirikiana nao. Juhudi kama hizi zinapanua msaada utolewao na jamii pana kwa shughuli za taasisi, ikiwemo asasi za umma na mawakala pamoja na viongozi wa kijadi. Kwa hakika, katika klasta ambako jitihada za jumuiya ya Kibahá'í zimefikia kiwango kikubwa cha kuthaminiwa na kuheshimiwa, ni jambo la kawaida kwa viongozi wenye mamlaka katika serikali za mitaa, huduma za umma, na asasi za kiraia kutafuta umaizi na ushirikiano. Waumini na Mabaraza ya Kiroho ya Mahali yanayowawakilisha wapo tayari kufanya kazi bega kwa bega na asasi za kijamii na wanakaribisha mawasiliano kama hayo, huku wakiwa macho kuepuka kujizongomeza katika siasa. Mara kwa mara, tumeona jinsi uhusiano wa marafiki na vyombo vya serikali za mitaa unavyopanuka zaidi ya ushirikiano na kukumbatia hisia ya dhamira ya pamoja, ikijikita juu ya maendeleo ya jamii—watu wakisonga mbele kama kitu kimoja. Katika maeneo mengi zaidi na zaidi, wakazi kwa ujumla wanalichukulia Baraza la Mahali kama lao vile vile, na huuona mwanga unaong'aa kutoka kwalo.

Mnamo 2021 tulisisitiza fursa zinazoweza kutokea pale shughuli za Kibahá'í zinapokita mizizi na kuenea mahali fulani, na ingawa mazingira ambako hili limetokea bado ni machache kwa idadi, ni jambo linaloongezeka kwa uthabiti. Haya ni maeneo maalum ndani ya klasta ambapo nguvu ya Imani ya ujengaji jumuiya ipo kwenye muonekano wake zaidi. Hapa, utendaji kazi wa Mpango unakuwa umejikita katika maisha ya kila siku ya watu kwa namna ambazo haziwezi kupimika kwa urahisi au kuelezewa kwa ukamilifu wake. Katika juhudi na

mashauriano yao ya pamoja, marafiki katika maeneo kama haya wanaendelea kushughulika na kukuza nafasi ambako watu hushauriana na kupeana maarifa, yanayotokana na sayansi na dini, na kupata njia za kutumia maarifa hayo kwa ajili ya maendeleo ya familia, elimu, shughuli za kiuchumi, afya ya umma, na michakato mingine ya msingi ya maisha ya jumuiya, wakijazwa ari mpya. Kwa kuzingatia athari pana za kinachotokea, neno "program ya ukuaji" halitendi tena haki kwa maendeleo kama haya. Ingawa katika sehemu zingine za klasta bado ukuaji unaweza kuwa katika hatua za awali, hapa, ambako kiwango cha ushiriki katika shughuli za Kibahá'í ni cha juu sana, uhalisia mpya huonekana kadiri uhusiano wa jumuiya ya Kibahá'í na jamii unavyokua. Mbingu angavu zinaita.

*

Katika mazingira ya kiasili, mchangano na uhusiano huleta msisimko na uhai mpya; vivyo hivyo, mchakato wa ujifunzaji unaoshamiri hutokana na miingiliano isiyohesabika rasmi na isiyo rasmi na sifa zake zinazoibuka. Mchakato huu hupambanuliwa kwa mtiririko usiokoma, mabadilishano yasiyokatishwa ya umaizi, tajiriba na mawazo miongoni mwa marafiki mashinani. Lakini hauishii hapo—unaendelea kukunjuka katika ngazi za kanda na kitaifa na zaidi, na ujifunzaji katika kila ngazi huchochewa na majadiliano yenye nguvu yanayofanyika katika nafasi zilizoandaliwa kwa ajili ya tafakari juu ya utendaji. Majadiliano haya hutumia ujifunzaji unaotokana na juhudi za jumuiya ya Kibahá'í kote ulimwenguni ndani ya muundo wa Mpango hali kadhalika matokeo yanayotokana na uchambuzi wa ruwaza inayojitokeza mahali husika. Bila shaka, majadiliano haya pia hubumbwa na asasi na mawakala wanaohudumu katika kila ngazi. Kwa kuwa watu binafsi, jumuiya na asasi zote zina mchango wa kutoa, ni asasi za Imani ndizo hatimaye zina jukumu la kukuza mfumo huu mzima wa ikolojia ya ujifunzaji. Hitaji muhimu sharti lihakikishe kwamba mipangilio ya kutosha ya kiasasi na isiyo rasmi sana imewekwa, ili kuuwezesha kustawi, na kwamba wote wanaohusika katika mchakato wa ujifunzaji wameunganishwa na uhusiano ya upendo yaliyojazwa ari ya unyenyekevu na ukarimu.

Uwezo wa asasi na mawakala kukuza mchakato wa ujifunzaji unahusiana kwa karibu na uwezo wao wa kusimamia kazi ifaavyo na kwa ufanisi. Kadiri hatua mbalimbali za kiutendaji katika eneo zinavyoongezeka na kuchangamana, Mabaraza ya Mahali yamekuwa na uwezo zaidi wa kukidhi hitaji la uratibu na upangaji. Mabaraza mara nyingi hushiriki jukumu hili na mawakala wa klasta, na kwa pamoja kuhakikisha kwamba ushauri, rasilimali na utiaji moyo vinaelekezwa pale vinapohitajika zaidi na kwamba mchakato wa ujifunzaji unaendelea kusonga mbele. Mawakala wa klasta hususan huhakikisha kwamba ujifunzaji uliopatikana katika eneo moja, au hata katika sehemu yake ndogo, unayanufaisha maeneo mengine ya klasta. Wakati huo huo, mbinu ya kupeana maarifa na umaizi ndani ya klasta unafanana na mbinu ya kupeana maarifa na umaizi baina ya klasta. Utoaji wa haraka wa msaada na kubadilishana tajiriba umewezekana kupitia maendeleo ya mipangilio ndani ya makundi ya klasta zinazokaribiana. Kwa kuwa sasa Halmashauri za Kibahá'í za Kanda au Kamati ya Ukuaji ya Kitaifa zimeanzishwa katika kila nchi, miundo ya kiasasi ipo kila mahali kwa ajili ya mchakato wa ukuaji kuendelezwa kimpangilio. Na katika ngazi ya kitaifa, wakati uzito na wingi wa kile kinachotokea hulazimu, Mabaraza ya Kitaifa yameunda miundo na nafasi fulani ili kusaidia kuyataarifu juu ya ujifunzaji unaopatikana. Kwa kawaida, muundo mpya usingeanzishwa vinginevyo mahitaji ya ukuaji yadai; hata hivyo, tunatazamia ninyi na wasaidizi wenu kuwa makini wakati mipangilio iliyopo katika ngazi yoyote ya jumuiya inapohitaji kubadilika ili kukidhi mahitaji ya ukuaji, na kisha, katika miingiliano yenu na asasi husika, kuhimiza kujitokeza kwa mipangilio mipya kwa namna ifaayo.

*

Pia tumebaini jinsi mipangilio ya kiutawala inayosaidia kazi ya taasisi ya mafunzo inavyobadilika kwa namna ambayo hulea mchakato wa ujifunzaji kuhusu uenezaji wa haraka wa program za taasisi zitolewazo kwa ubora unaohitajika. Katika hatua za awali, mipangilio hii inakuwa rahisi sana, lakini kadiri idadi ya wale walioko katika nguzo wakihudumu kama wakufunzi, wahuishaji na walimu wa madarasa ya watoto iongezekavyo, hitaji la wao kujihusisha kikamilifu katika mchakato wa ujifunzaji wa pamoja linakuwa la haraka zaidi. Ni muhimu kwamba waweze kudumisha mazungumzo ya mara kwa mara baina yao, kutafakari pamoja katika makundi, na kusaidiana katika utendaji. Ruwaza hizi za mwingiliano hutokea kwa urahisi zaidi pale marafiki wanaoshiriki wanaposindikizwa kwa ufanisi na waratibu na waratibu-wenza wanaowasaidia. Bila shaka, waratibu wenyewe pia wanahitaji kuinuliwa katika kila klasta na kusaidiwa kukuza uwezo wao kadiri muda upitavyo, na hili kwa kawaida ni jukumu la waratibu wa taasisi wa kanda au kitaifa, ambao jitihada zao, kwa upande wao, zinazidi kuimarishwa na timu za marafiki kwa kila program ya kielimu. Katika miaka minne iliyopita, timu hizi zimefanya mengi kuwasaidia waratibu wa kanda na kitaifa kuandaa semina zinazochunguza kwa kina maudhui ya programu, na hivyo kuwezesha nyenzo za taasisi kufunzwa kwa idadi kubwa zaidi ya watu, kiubunifu, kiunyumbulifu na kwa uharaka uongezekao daima—lakini bila kuathiri vipengele vya kimsingi vya program.

Wakati wote, tajiriba na umaizi unaojitokeza kutokana na yale ambayo taasisi inajifunza hukusanywa, kuchambuliwa na kusambazwa. Kazi hii inanufaika kwa kiasi kikubwa kutokana na mikusanyiko ya ushauriano, inayoitishwa kipindi hadi kipindi na taasisi, ambayo huwaleta pamoja Washauri Wasaidizi, wawakilishi wa Halmashauri ya Kibahá'í ya Kanda au Kamati ya Ukuaji ya Kitaifa, rasilimali watu kutoka kituo cha ujifunzaji, na watu wengine ambao tajiriba yao imekuwa rasilimali inayothamaniwa. Mikutano ya kundi hili la wanaoshirikiana husaidia kuimarisha uhusiano wa taasisi, asasi na mawakala wengine, kuhakikisha kwamba mchakato wake wa ujifunzaji hukunjuka ndani ya muktadha mpana wa kujifunza kuhusu mchakato wa ukuaji kwa jumla. Bodi ya taasisi pia huimarisha vipengele vingine vyote vya taasisi, ikiwemo uwezo wake wa kiutawala, ili iweze kudumisha mfumo unaozidi kuwa tata wa elimu ya kiroho. Na takriban taasisi zote sasa zimepangwa katika makundi ili kurahisisha mtiririko wa yote mawili; msaada wa kivitendo na umaizi wenye thamani; maendeleo ya mitandao hii yameonekana kuwa mkakati muhimu kwa ajili ya taasisi kusonga mbele kwa haraka.

*

Imekuwa ikituletea furaha kuona roho zilizowashwa tulizozielezea katika ujumbe wetu kwa kongamano lenu la 2021, katika klasta baada ya klasta na kwa idadi kubwa zaidi na zaidi, zikitekeleza Mpango kwa moyo wa kujitoa kabisa na, muhimu zaidi, kujidhatiti kwenye mchakato wa ujifunzaji. Huu ndio msingi wa uhakika kabisa kwa ajili ya maendeleo yanayohitajika kufanywa katika awamu ya pili ya Mpango.

Michakato inayokunjuka katika Mpango bila shaka inaleta athari ya kina ya mabadiliko kwa mtu binafsi. Tunachoshuhudia ni marafiki wenye shauku wakijifunza jinsi ya kupatanisha kwa karibu zaidi jitihada zao na Mapenzi ya Mungu. Kupitia kushiriki katika muundo wa kiutendaji wa Mpango, watu binafsi wanagundua njia za kuboresha maisha—katika sura zake zote—kwao wenyewe, kwa watoto wao, kwa familia zao pana, na kwa jumuiya yao. Ni ufahamu wao wa juu kabisa wa kiroho ndio unaowaongoza kwenye maisha yenye kusudi na maana, maisha yaliyowekwa wakfu kwa ajili ya kukuza uwezo wao wa kiasi waliopewa na Mungu na kufanya

kazi kwa bidii kwa ajili ya mabadiliko ya jamii. Wanatambua thamani ya elimu katika kuchochea maendeleo, wamejidhatiti kwa ajili ya uzalishwaji wake, na kuitoa kwa uhuru na kwa unyenyekevu. Ujifunzaji ni tabia ya akili kwao, mwelekeo katika kila wanachokifanya. Katika kila uso wanamuona mtafutaji mwenzao wa ukweli. Wanajitoa kikamilifu kwa ajili ya maendeleo ya kiroho, kiakili, na kimwili ya watu. Hawaondolewi katika njia kwa usumbufu usiokoma wa dunia. Kwa uthabiti wanasonga mbele wakiwa watulivu, wavumilivu na wastahimilivu, wakiapa kwa jitihada za muda mrefu. Na katika kuungana na wengine wengi, wanajenga makao ya amani.

Imeonekana mara kwa mara kwamba kadiri watu binafsi wanavyokuwa na ufahamu zaidi wa umuhimu wa ruwaza pana ya shughuli katika mazingira yao, wanakuwa tayari kutoa muda na msukumo wenye ubunifu ili kuiendeleza zaidi. Zaidi kwa ujumla, waumini pia husaidia jumuiya yao kwa kuchangia Mfuko na kutoa aina zingine za rasilimali za kimwili. Wakati waumini wote hutoa michango ya aina hii, kwa baadhi ya waumini wenye uwezo, hii ni njia ya kuuendeleza Mpango ambayo wao hususan wapo katika nafasi nzuri zaidi kuitumia. Aina yoyote ya huduma aitoayo mtu, kwa upande mmoja, inatokana na mwingiliano wa kipekee kati ya mahitaji ya Imani, na kwa upande mwingine, fursa zitokanazo na hali za kila mtu na dhabihu ambazo yeye huchagua kuitoa.

Na waumini wanazidi kuthamini heshima ya kuwa na uwezo wa kuifahamisha roho kuhusu ujumbe wa Bahá'u'lláh—na, zaidi ya hili, kuisaidia kwa upendo roho ambayo husimama kwenye milango ya Imani kuingia ndani. Mnamo 2021 tulivuta nadhari kwenye wakati huu adhimu katika safari ya kiroho. Tumebaini kwa shauku kwamba, tangu wakati huo, marafiki katika maeneo mengi wameelekeza umakinifu juu ya namna ya kutambua ni wakati gani mji wa moyo unakuwa wazi, na juu ya mazungumzo yanayoongozea kwenye wakati huu na yale yanayoufuatia. Bado kuna mengi ya kujifunza katika jambo hili, kuhusu jinsi ya kutambua upokevu katika mazingira tofauti tofauti na jinsi ya kutambua ni wakati gani tayari umekomaa kuwa imani.

Kwa kutazama nyuma katika maisha ya mtu, hakuna furaha na faraja kubwa zaidi kuliko kujua kwamba yalitumika katika utambuzi wa kina wa tiba takatifu, kwamba hakuna juhudi iliyoachwa kutoa tiba hiyo kwa roho pokevu, na kwamba katika miaka hiyo ipitayo upesi wakati fursa ilipokuwa mkononi, hata katikati ya matatizo, kila nafasi ilitumiwa kuitikia hitaji kubwa la jamii ya binadamu. Kwa ari na shauku tunamsihi Bahá'u'lláh, kila wakati tunapofika mbele ya Kizingiti Chake, kwa ajili ya mafanikio ya marafiki wote.

Nyumba ya Haki ya Ulimwengu